BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Tisa – Tarehe 27 Mei, 2024

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2024/2025.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka 2024/2025.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

211. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Tathmini iko vipi juu ya ongezeko la vijana wanaotumia madawa ya kulevya kupitia vijiji vyetu mbali mbali hususan kwenye ukanda wa sekta za mahoteli ya kitalii Zanzibar.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

244. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tathmini ya ongezeko la vitendo vya rushwa iko vipi kwa sasa.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

216. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

(a) Je, 'Corporate Social Responsibility' ni fursa au ni haki kwa wananchi.

(b) Kwa nini wawekezaji wengi hawatekelezi ipasavyo utaratibu huu.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

60. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Awamu ya Nane chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kipindi kifupi imefanya kazi kubwa ya kuimarisha miundombinu ya michezo nchini na matunda yake yanaonekana dhahiri. Kwa kuwa nchi yetu imepata bahati ya kuzalisha vipaji vya michezo mbali mbali hasa vya mpira wa miguu kupitia ligi za watoto (juvenile).

(a) Kwa nini ligi za watoto zimekosa hamasa na mvuto kama ilivyokuwa zamani, wakati hivi sasa tuna viwanja vizuri vya michezo.

(b) Je, Serikali kwa kushirikiana na ZFF wana mkakati gani wa kutoa ufadhili kwa ligi za watoto Unguja na Pemba ili kuimarisha ukuzaji wa vipaji vya watoto hao.

(c) Mpaka hivi sasa utaratibu wa kuendesha ligi za watoto unafanyika vipi na changamoto gani zinaukabili uendeshaji huo.

**Wizara ya Afya:**

162. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Pamoja na juhudi mbali mbali zinazochukuliwa na Wizara yako katika kuhakikisha wananchi wetu wanaepukana na maradhi mbali mbali, tatizo la maradhi ya ugumba bado limekuwa sugu kwa wananchi wetu.

Je, Wizara yako imefanya tathmini yoyote kuhusiana na ongezeko la tatizo la ugumba unaotokana na maradhi mbali mbali hapa Zanzibar.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

268. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapatia mbolea wakulima wa Wilaya ya Kati, ili waondokane na changamoto ya kupatikana kwa mbolea

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

251. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

(a) Ni asilimia ngapi ya wananchi wa Zanzibar kwa sasa wanatumia simu za mkononi na asilimia ngapi wanatumia simu za mezani hadi sasa.

(b) Ni asilimia ngapi ya wananchi wanatumia huduma za mawasiliano ya kimtandao mpaka sasa.

(c) Kwa kiasi gani huduma za matumizi ya simu za mkononi na mawasiliano ya kimtandao zinarahisisha au kuleta changamoto katika maendeleo ya jamii hapa Zanzibar.

## <u>Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

90. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Naipongeza Serikali kwa mkakati mzuri iliyokuwa nao wa kutoa ruzuku kwa skuli za sekondari kwa lengo la kuongeza ufanisi na ufaulu wa wanafunzi katika nchi yetu. Pamoja na utoaji huu wa ruzuku uliozifaidisha skuli zetu na kuziwezesha kujiendesha, kuna masikitiko kuwa jambo hili zuri limesita hivi karibuni, hali inayozifanya skuli nyingi kuwa katika hali isiyoridhisha ya uendeshaji.

(a) Je, ni ipi idadi kamili ya skuli zilizowahi kunufaika na ruzuku kupitia programu hii ya Serikali.

(b) Je, ni vipi vyanzo vya ruzuku hizi zilizokuwa zikitolewa na kwa nini hivi sasa zimesita kutolewa.

(c) Je, Serikali ina mpango gani endelevu na wa muda mrefu wa kuendelea kuzipatia ruzuku skuli za Sekondari.

94. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Skuli ya Makongeni katika jimbo la Mtambwe ilipokea ufadhili wa ujenzi wa madarasa matatu (3) kupitia mfuko wa UVIKO 19 kwa mujibu wa mchoro waliopatiwa awali. Hata hivyo, utekelezaji wa mpango huo haukufanyika kikamilifu, na matokeo yake ilipelekea kumalizwa kwa darasa moja (1) tu ambalo tayari lilikuwa limejengwa kwa jitihada za wananchi:

(a) Je, Serikali inalitambua jambo hili na ni hatua gani imechukua kulitatua.

(b) Je, ni sababu gani iliyosababisha kubadilishwa kwa mchoro wa awali wa ujenzi wa madarasa matatu (3) kupitia UVIKO 19 katika skuli hii.

(c) Kufuatia uhaba mkubwa wa madarasa katika skuli hiyo uliosababisha watoto 200 kusomea katika darasa moja, ni ipi juhudi ya Serikali katika kulitatua tatizo hili kwa haraka.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

174. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kisiwa cha Uzi ni miongoni mwa visiwa vyenye vivutio vikubwa sana na vizuri vya utalii hapa Zanzibar.

(a) Kwa namna gani suala la uharibifu wa mazingira ikiwemo ukataji wa mikoko katika kisiwa cha Uzi linaathiri shughuli za utalii katika kisiwa hicho.

(b) Je, kwa kiasi gani utalii unaweza kuwa miongoni mwa njia mbadala ya kuwasaidia wananchi wa kisiwa hiki kuondokana na njia za kiuchumi wanazozitumia hivi sasa, ikiwa ni pamoja na kukata mikoko.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa mwaka 2024/2025.

**Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2024/2025.

**Zanzibar,**
**27 Mei, 2024.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**